# Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo

## 1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 JULAI, 2025

### 1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA TAREHE 21-30 JUNI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kudhoofika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa ukandamvua kuelekea kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Makutano ya upepo katika maeneo yanayozunguka Ukanda wa Ziwa Victoria yaliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo hayo. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusinimashariki mwa Afrika) liliendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii ilisababisha uwepo wa mgandamizo mkubwa wa hewa ambao uliongeza kasi ya upepo uvumao kutoka baharini kuelekea pwani ya Afrika Mashariki.

### 1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-30 JUNI, 2025

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua katika maeneo machache ya ukanda wa ziwa Viktoria na ukanda wa Pwani pamoja na vipindi vya upepo mkali na mawimbi makubwa katika maeneo hayo.

## 2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 JULAI, 2025

### 2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 JULAI, 2025

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika. Hali hii inatarajiwa kudumisha mwenendo wa ukandamvua kuelekea kaskazini zaidi, nje ya nchi yetu. Kwa upande mwingine Joto la bahari katika eneo la kusini-magharibi mwa Bahari ya Hindi (Kusinimashariki mwa Afrika) linatarajiwa kuendelea kuwa la chini ya wastani. Hali hii

inatarajiwa kusababisha uwepo wa mgandamizo mkubwa wa hewa ambao unatarajiwa kuongeza kasi ya upepo uvumao kutoka baharini kuelekea pwani ya Afrika Mashariki.

**2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 JULAI, 2025**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua nyepesi na upepo mkali vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Hali ya ukavu inatarajiwa.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Hali ya ukavu kwa ujumla na vipindi upepo mkali vinatarajiwa.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

Imetolewa na;

***MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA***

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz